

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MKOA NA SERIKALI ZA MITAA
HALMASHAURI YA WILAYA YA LUDEWA**



Septemba 03, 2022

**MKOA WA NJOMBE WASHIRIKI KILELE CHA SHEREHE ZA KIZIMKAZI FESTIVAL
ZANZIBAR**

Mkuu wa Mkoa wa Njombe Mhe. Anthony Mtaka pamoja na Katibu Tawala wa Mkoa wa Njombe Bi. Judica Omari wakiambatana na Wakuu wa Wilaya za Mkoa wa Njombe leo Septemba 03, 2022 wamehudhulia mualiko wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Samia Suluhu Hassan uliokuwa ukiadhimisha siku ya KIZIMKAZI FESTIVAL katika Mkoa wa Kusini Unguja katika kijiji cha Kizimkazi Zanzibar.

Aidha Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Ludewa Ndg. Sunday Deogratias akiwawakilisha Wakurugenzi wote nchini Tanzania amehudhulia sambamba na Katibu Tawala wa Wilaya ya Ludewa Bwn. Linus Malamba pamoja na Afisa Habari wa Halmashauri ya Wilaya ya Ludewa Ndg. Chrispin Kalinga wakiambatana na Ngoma ya asili ya Mganda kutoka Wilaya ya Ludewa nao wameshiriki.

Sambamba na hayo Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Samia Suluhu Hassan ameupongeza Mkoa wa Njombe na kuwashukuru viongozi wote wa mkoa huo kwakushiriki siku hiyo muhimu katika Mkoa wa Kusini Unguja.

A handwritten signature in blue ink, appearing to read 'Chrispin B. Kalinga'.

Chrispin B. Kalinga
Afisa Habari na Mawasiliano Serikalini
Halmashauri (W) Ludewa.